

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TANO**

**KIKAO CHA TATU**

**04 NOVEMBA, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA TATU – TAREHE 04 NOVEMBA, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

31. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY  
(MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja la Gunyoda ambalo linaunganisha Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu hususani Tarafa ya Mang'ola kwenye mashamba ya Vitunguu.

**32. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Wodi za kulaza Wagonjwa pamoja na kupeleka mashine ya X-ray katika Kituo cha Afya Itobo kilichopo Jimbo la Bukene.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**33. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**



Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Tanzania ina idadi ya Watu takribani milioni hamsini na tano wenye madaraja tofauti ya uchumi;

Je, katika idadi hiyo Tanzania ina Mabilionea wangapi.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **34. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni kwa nini Serikali isiingie makubaliano na Chuo cha Ufundi Lugarawa kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Njombe kwa kupeleka Walimu, vifaa na fedha za ruzuku ili Wanaludewa na Wananjombe wapate mafunzo wakati ujenzi wa Chuo cha VETA Shaurimoyo ukisubiriwa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **35. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kugharamia matengenezo ya Reli ya TAZARA ambayo miundombinu yake imechakaa na ni muhimu

sana kwa Uchumi wa Tanzania na hata kwa nchi jirani za SADC.

### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

#### **36. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Benki ya Wavuvi nchini.

### **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

#### **37. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuwajumuisha Wenyeviti wa Halmashauri na Wabunge kwenye Kamati za kujadili na kupitisha maombi ya Wavunaji wa mali za misitu kwenye Wilaya zetu nchini.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **38. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali imepanga kuanza kukarabati majengo ya Kituo cha Polisi Makunduchi.

### **III. KAMATI YA MIPANGO:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, Kujadili na Kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
04 NOVEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**